# Uhuru na Amani

GAZETI LA KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA TOLEO LA 1 2018 Bei Sh. 1,000/-

KKKT

ELCT





## YALIYOMO NDANI

TOLEO MAALUMU

KKKT yakaribisha Mkutano wa Misioni na Uinjilisti wa Dunia


- Kutoka Achimota hadi Arusha
- Safari ya misioni kiekumene
- Afrika ni kinara wa misioni
- "Tumwabudu Mungu Wetu" chawasili
- Ni Dkt. Mwaikali Dayosisi ya Konde
- Matengenezo na kujenga umoja
- Viongozi muangaze kama nuru
- Wakristo msiwe vuguvugu


TOLEO LA 1 2018 ISSN 0856 - 1214 Na. 1 Vol. 118

# Tuombee mkutano wa misioni ya dunia

**KKKT**

**ELCT**



**Naibu Katibu Mkuu wa Misioni na Uinjilisti KKKT, Mchg. Lazaro Rohho**

Idara ya Misioni na Uinjilisti KKKT Inaona heshima kubwa kwa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kihistoria wa Misioni duniani. Tarehe za Mkutano 8 - 13 Machi, 2018

Wakristo watu wote mnaalikwa kuombea mkutano kabla na wakati wajumbe wakiwa Arusha kwa ajili ya mkutano huo. Neno kuu la Mkutano huo: ***"Kuenenda kwa Roho: Wito wa kuwa wafuasi wa mabadiliko"*** Wagalatia 5: 25

OIKOUMENE World Council of Churches


**Uhuru na Amani 2018**

# "Tumwabudu Mungu Wetu" kinapatikana

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) linapenda kuwatangazia washarika wote kwamba toleo jipya la kitabu:

**"Tumwabudu Mungu Wetu"**

chenye umbo dogo na mwonekano mpya, sasa kinapatikana. Nakala moja ni **Sh. 12,000/-**




**Mawasiliano:**

**E-mail:** lmrohho@elct.or.tz

**Simu:** +255 766 288 887

**Tangazo limetolewa na:**

Naibu Katibu Mkuu Misioni na Uinjilisti, KKKT,
Mchg. Lazaro Rohho.

**Uhuru na Amani**

Uhuru na Amani
Gazeti la KKKT
Toleo la 1, 2018
Na. 1 Vol. 118
ISSN 0856 - 1214

Uhuru na Amani ni Gazeti la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Hutayarishwa na Kitengo cha Mawasiliano, KKKT.

Maoni yaliyomo katika makala zinazochapishwa ni ya mwandishi anayehusika na wala hayawakilishi mawazo ya Kanisa ama mhariri isipokuwa pale ambapo imetamkwa wazi. Ukiwa na maoni, ushauri, makala au maswali mwandikie:

**Mhariri**
**Uhuru na Amani**
**S.L.P. 3033**
**ARUSHA**
**Barua pepe:** elobulu@elct.or.tz
**Sms** WhatsApp Skype kwa Mhariri: +255-754-482-285
**Fungua Tovuti ya KKKT:** http://www.elct.org/

**MHARIRI**
**Elizabeth Lobulu**

Limepigwa Chapa na:
**Perfect Printers Ltd.**
S.l.P 1487 Arusha +255 764 283 996
perfect@perfectprinters.co.tz

Newspaper Design & Typesetting:
**Elizabeth Lobulu**

**Wachangiaji wa Makala:**

Dkt. Agnes Abuom
Metropolitan Dkt. Mor Geevarghese Coorilos
Mch. Dkt. Olav Fykse Tveit
Mch. Jooseop Keum
Dkt. Rogate Mshana
Askofu Mkuu Dkt. Musa Panti Filibus
Mchg. Dkt. Ipyana Mwamugobole
Shemeji Melayeki

**PICHA YA JALADA:**

Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo (kushoto), na Mwenyekiti wa vikao vya Kamati Kuu, WCC, Dkt. Agnes Abuom.

# MAONI YA MHARIRI

## Tuenende kwa Roho

Baraza la Makanisa Duniani (WCC) limeandaa mkutano wa Misioni wa Dunia utakaofanyika Tanzania 8 hadi 13 Machi, 2018 Ngurdoto Mountain Lodge, nje kidogo ya jiji la Arusha. Kauli mbiu - *"Kuenenda kwa Roho: Wito wa kuwa wafuasi wa mabadiliko."*

Kanisa la Kiiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ambalo ni mwanachama wa Baraza hilo limepokea kwa mikono miwili heshima ya kuwa mwenyeji wa mkutano huo wa kimataifa ambao unahusisha madhehebu mbalimbali ya Kikristo.

Mkutano wa kwanza wa Kimataifa wa Misioni ulifanyika Edinburgh, Uingereza mwaka 1910 na kuhudhuriwa na washiriki 1,200. Wakati huo waliohudhuria ni wawakilishi wa vyama vya misioni. Moja ya mambo muhimu kutokana na mkutano huo ni kuundwa kwa Baraza la Kimataifa la Kimisionari (International Missionary Council - IMC).

Mkutano huo ulitaka kuweka misisitizo wa misioni kiekumene. Mwaka 1958 Mkutano wa Misioni ya Dunia ulifanyika kwa mara ya kwanza Afrika.

Mwaka 1961, IMC iliunganishwa na WCC na kuanza kuandaa Mikutano ya Misioni ya Dunia katikati ya mihula ya mikutano mikuu ya WCC.

KKKT inamshukuru sana Mungu kwa kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Pili ya Misioni wa Dunia barani Afrika.

Mkuu wa KKKT, Askofu Fredrick Shoo ameomba washarika na watu wote waombee mkutano.

Karibuni mjisomee zaidi katika toleo hili maalum kwa ajili mkutano huo. Katika kurasa za mwamzo utajisomea maelezo kuhusu mkutano huu ambao hufanyika mara moja kila miaka 10. Na Mkutano wa Arusha ni wa 14.

# Mkutano wa Misioni wa Dunia kufanyika Arusha

Mkutano wa Misioni wa Dunia ulioandaliwa na Baraza la Makanisa Duniani (WCC) utafanyika Arusha 8 hadi 13 Machi, 2018.

Katibu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Bw. Brighton Killewa, amesema hivi karibuni kwamba inatarajiwa washiriki 1,200 toka pande zote za dunia watahudhuria mkutano huo utakaofanyika hoteli ya Ngurdoto, Arusha. Mara ya kwanza katika bara la Afrika mkutano kama huo ulifanyika nchini Ghana katika mji unaoitwa Achimota mwaka 1958.



Bw. Brighton Killewa, Katibu Mkuu wa KKKT.

## Dkt. Abuom aeleza dhana ya mkutano

**DKT. AGNES ABUOM, kutoka Kanisa la Anglican Kenya, ni Mwenyekiti wa vikao vya Kamati Kuu ya Baraza la Makanisa Duniani (WCC). Yeye ameandika dibaji ya kitabu cha rejea kilichotoka kwa ajili ya Mkutano wa Misioni wa Dunia 8 – 13 Machi, 2018. Haya ni baadhi ya mawazo yake baada ya kuhojiwa na MWANDISHI WA WCC.**

Dkt. Abuom anasema tafiti mbalimbali zinaonesha kwa sasa Afrika na nchi za kusini ndio kitovu cha ukiristo duniani. Na kwa mara ya kwanza Afrika ilikuwa mwenyeji wa mkutano wa Misioni wa Dunia (CWME) miaka 60 iliyopita. Mkutano huo ulifanyika katika mji wa Achimota, Ghana, mwaka 1958.

Alisema kwa kurudi Afrika eneo la mkutano litatoa fursa kuona kwa uhalisia maumivu, hasira ambayo ni mambo yanayozonga jamii ya Afrika. Pia kusheherekea na hata kuona changamoto za kazi za misioni kiekumene siku hizi. Mikutano ya misioni hufanyika kila miaka 10 na akaeleza kwamba hata mikutano iliyotangulia nayo ilikabili masuala ya wakati wake kama ubaguzi wa rangi, amani, ushirikiano na upatanisho.

Akigusia kauli mbiu ya mkutano inayosema "Kuenenda katika Roho: Wito wa kuwa wafuasi wa mabadiliko", alisema kupitia mkutano huu kwa mara nyingine Afrika inapaswa kurudi na kujipanga vyema zaidi katika suala la imani ya Kristo. Pia kujiuliza je wito wa ufuasi wa mabadiliko ni katika kupewa uwezo ya kubalilisha maisha ya watu duniani kote au ni kuwaacha watu wengine waendelee kuwa watumwa?

**Swali: Kwa nini mkutano huu umefanyika Afrika?**

**Dkt. Abuom:** Mahali pa mkutano panatukumbusha makutano ya imani mbalimbali barani Afrika: Ukristo, Uisalamu na dini za jadi za Kiafrika. Ni mahali panapohuisha roho ya kutaka mabadiliko na shauku ya kuwa na dunia yenye mtazamo mbadala, unaolenga kuwa na mfumo wa kiuchumi na kisiasa ulio rafiki kwa watu, uliyokolezwa na tunu zinazothamini uhai na mambo ya kiroho. (Chanzo: WCC)

Ukitaka maelezo zaidi fungua uk. wa 8.



Dkt. Agnes Abuom,
Mwenyekiti vikao vya Kamati Kuu WCC.

Nembo ya Mkutano wa Misioni wa Dunia 2018

## Kitabu cha Historia ya misioni Afrika chatolewa

Baraza la Makanisa Duniani (WCC) limetoa kitabu cha rejea kuhusu historia ya kazi ya Misioni barani Afrika na historia ya kuanzishwa kwa Kamisheni ya Misioni hadi kuwa Mkutano wa Misioni wa dunia (CWME).

Kitabu pamoja na mambo mengine kimeeleza kuhusu safari ya misioni kiekumene barani Afrika. Makala katika kitabu zimeandikwa na wasomi na watheolojia waliobobea kutoka madhehebu mbalimbali. Kitabu hicho kinaitwa *"From Achimota to Arusha: An Ecumenical Journey of Mission in Africa."*

Namba ya kitabu ni: ISBN 978-2-8254-1700-3

**Kwa maelezo zaidi fungua tovuti:** http://publications.oikoumene.org/

OIKOUMENE World Council of Churches

KKKT

ELCT

# TOLEO MAALUM

## Mkutano wa Misioni wa Dunia

KAULI MBIU - *Kuenenda kwa Roho: Wito wa kuwa wafuasi wa mabadiliko*

### Shabaha za Mkutano

- Kuwezesha mkutano kuwa jamii hai inayozingatia ufuasi wa mabadiliko
- Kuhimiza washiriki wapate maono mapya yatakayowatia nguvu ili kujifunza wito wa Mungu leo
- Kushiriki nguvu ya kiroho itakayotia nia ya mabadiliko kuhuisha jumuia na jamii zetu
- Kuhakikisha ipo fursa salama ya kutafakari, kupashana habari na kuendeleza maongezi
- Kutiana hamasa kuhusu masuala ya misioni kiekumene kwa kuwaza na kwa vitendo
- Kusherehekea umoja wetu katika Mungu wa utatu na katika tofauti zetu za kiuungu
- Kuwezesha washiriki wajitoe kwa dhati kama wafuasi wa mabadiliko katika muktadha wao kutokana na maadili kama itikio la Mkutano wa Arusha.

(CHANZO: WCC)

# Karibuni Afrika na Tanzania

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) linaona limepewa heshima na upendeleo kuwa mwenyeji wa Mkutano huu muhimu wa Misioni wa Dunia utakaofanyika Arusha chini ya kauli mbiu - ***"Kuenenda kwa Roho: Wito wa kuwa wafuasi wa mabadiliko."***

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) aliyasema hayo katika salamu zake kwa wajumbe ambazo ziko katika kitabu cha mwongozo wa wajumbe wa mkutano huo utakaofanyika 8 hadi 13 Machi 2018.

Kwa kuwa mkutano huo unafanyika Afrika kwa mara ya pili alisema: "Karibuni Afrika na Tanzania." (CHANZO: WCC)



**Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo, Mkuu wa KKKT.**

# Salamu za Katibu Mkuu WCC

Kwa kuwa zaidi ya wageni 1,000 watawasili jijini Arusha kuhudhuria Mkutano wa Misioni na Uinjilisti wa Dunia, napenda kuwashukuru watu wa Arusha na ndugu zetu Wakristo kwa kutukaribisha na kwa kushiriki matukio ya sherehe na warsha katika mkutano.

Mkutano huu wa Misioni na Uinjilisti ni miongoni mwa alama muhimu katika hija yetu ya kiekumene katika mwaka huu ambapo Baraza la Makanisa Duniani (World Council of Churches - WCC) limefikisha miaka 70 tangu lianzishwe.

Kamisheni iliyoandaa mkutano huu ina umri mkubwa kuliko umri wa WCC, na chimbuko lake linatokana na jitihada ya maono ya wamisionari ya zaidi ya miaka 100 iliyopita, iliyokusudia kuondoa kashfa ya utengano miongoni mwa Wakristo na kufikiri kwa upya wajibu na masuala ya Misioni.

Leo hii tunaichukulia Misioni kwa njia tofauti kabisa. Misioni kwa Mkristo siyo kule kuongoa, au *kutafuta samaki wa kumvua.* Bali ni kwa Wakristo kujifunza toka kwa wale wanaoishi pembezoni mwa jamii. Ni kule kuwahudumia wale ambao wengine wamewasahau, wamewapuuza au wanao nyanyaswa. Ni kule kuamua kusaidia wengine nao wafaidike na zawadi ya Mungu ya maisha. Hivyo misioni inahusu mabadiliko: Misioni ya Mungu itubadilishe sisi na makanisa yetu na jamii yetu na dunia iwe himaya ya Mungu na ufalme wa upendo.

Tunakuja Arusha kwa upendo na mategemeo. Tunaheshimu uwepo wenu na kwa kukubali kushirikiana nasi katika umoja wenu ili kupata mwelekeo wa siku zijazo wa Misioni ya Kanisa kwa wakati wetu. Tunaona tumependelewa kwa kushirikiana nasi katika kusudi hili takatifu.

Olav Fykse Tveit
Katibu Mkuu,
Baraza la Makanisa Duniani.
CHANZO: WCC



**Mch. Dkt. Olav Fykse Tveit, Katibu Mkuu wa Baraza la Makanisa Duniani (WCC).**

## Fahamu jukumu la Baraza la Makanisa Duniani

Baraza la Makanisa Duniani (World Council of Churches - WCC) ni jumuiya ya kiekumene ya makanisa iliyoundwa mwaka 1948. Hadi sasa inajumuisha makanisa 348 ya Kilutheri, Orthodox, Anglikana, Baptist, Methodist, Reformed na makanisa mengine. Kwa pamoja jumuiya hiyo ina wakristo milioni 550 katika nchi 120. Pia inashirikiana na Kanisa Katoliki.

Jukumu kuu la jumuiya hiyo ni kusaidia kujenga umoja wa Wakristo katika imani, ushuhuda na huduma ili kuleta haki na amani duniani.

Japo makanisa yaliyoanzisha jumuiya hiyo ni kutoka Ulaya na Amerika ya Kaskazini, kwa sasa makanisa mengi wanachama ni kutoka Afrika, Asia, Caribbean, Latin America, Mashariki ya Kati na Pacific.

**Kwa taarifa zaidi fungua tovuti: www.oikoumene.org/press**

Na Mch. Jooseop Keum

# Afrika haikuwakilishwa vizuri Achimota




**Mch. Jooseop Keum,**
**Mkurugenzi wa Kamisheni ya Misioni na Uinjilisti ya Dunia, WCC.**

Mara ya kwanza Mkutano wa Misioni wa Dunia ulifanyika mwaka 1958 mjini Achimota, Ghana. Hakika jambo hili kwa wakati huo lilivunja rekodi ya kihistoria, lakini dosari kubwa ni kwamba ushiriki wa watu toka barani Afrika ulikuwa mdogo sana.

Inawezekana hali hiyo ilitokana na mfarakano uliokuwepo wa vyama vya kimisionari Afrika na kwa kuwa baadhi yake havikuwa na uhusiano na Baraza la Kimataifa la Kimisionari - ***International Missionary Council (IMC)***.

Hata hivyo Afrika sasa imesonga mbele licha ya malalamiko na changamoto za kazi za umisionari wakati wa ukoloni na biashara ya utumwa. Tunathamini mchango wa wamisionari ambao waliacha maisha waliyozoea na kuamua kufika Afrika kueneza Injili. Baadhi yao walikufa kutokana na maambukizi ya magonjwa. Baadhi waliishi katika hali duni isiyoweza kuelezeka. Kazi yao njema kamwe haijasahaulika hadi leo miongoni mwa Waafrika walio wengi.

Ni jambo dhahiri kwamba Afrika ni bara la watu wapenda dini.

Hivyo, miongoni mwa shabaha ni kufanya mkutano uwe ni wa Kiafrika kwa maana:

• ile roho na vionjo vya Kiafrika katika muziki, na sanaa itatawala anga la eneo la mkutano na wakati wa vipindi vya Ibada za pamoja;

• Washiriki wa mkutano itabidi wasome alama za nyakati na kushughulikia mambo yanayokabili Waafrika na nchi zao – alama ambazo ni tishio na zile za kutia matumaini;

• Mkutano utachota baraka toka katika eneo moja wapo lililo imara kwa vile Waafrika wamejaliwa msisimko mkubwa na uchangamfu katika masuala ya *imani ya Kikristo* duniani kwa uhai wa kiroho na kuhuisha maisha;

• Mkutano utaonesha waziwazi mchango na mtazamo wa Afrika kwa kulinganisha na mitizamo iliyopo na kubainisha uelewa wake kuhusu Misioni na kuongoza jinsi ya kuenenda katika masuala ya theologia ya Misoni na uhalisia wake kwa siku zijazo; na

• Watoa mada wengi watakaoongea katika vipindi vya pamoja na wakati wa ibada ni Waafrika na kutakuwa na washiriki wanaume, wanawake na vijana Waafrika.

Ni muhimu kuwa na maelezo kuhusu yale yaliyofanyika Achimota na yale ya mkutano wa Arusha. Maelezo kama hayo ndio yanayoonesha alama zilizowekwa katika ufuasi wa Kikristo, ushuhuda wa imani na kazi ya ekumene inayofanywa na Afrika na Waafrika.

Ni matumaini yangu kwamba hazina iliyopo katika maandiko itaanzisha hamu kwa vijana wadogo wa Kikristo ili na wao wakubali kwa moyo wa dhati kuanza kushuhudia wengine ili kutimiza lengo la Misioni katika jamii ya wasiyomwamini Mungu barani Afrika.

**Sehemu ya mada hii imetokana na Utangulizi wa Kitabu cha "*Achimota to Arusha*" ulioandikwa na Mch. Jooseop Keum akishirikiana na Mch. Lesmore Gibson Ezekiel Mhadhiri wa Catholic University of Eastern Africa, Nairobi. (CHANZO: WCC)**

## RATIBA

Mkutano wa Misioni wa Dunia kila siku asubuhi, mchana na jioni kutakuwa na vipindi vya sala za pamoja isipokuwa siku ya Jumapili ambapo wajumbe wamepangiwa kushiriki Ibada katika makanisa ya Arusha na mkoa wa Kilimanjaro.

## KAULI MBIU ZA SIKU

Vipindi vya pamoja wakati wa Mkutano wa Misioni wa Dunia vitakuwa na kauli mbiu kama ifuatavyo:

08/03/2018
● KUENENDA PAMOJA: Kusherehekea na Kuomboleza
09/03/2018
● KUMFUATA YESU: Kuwa wafuasi
10/3/2018
● KUWA WAFUASI: Kuleta mabadiliko duniani
11/3/2018
● KULETA MABADILIKO DUNIANI: Kuwapa wafuasi nyenzo
12/3/2018
● KUWAPA WAFUASI NYENZO: Kuukubali Msalaba

## WARSHA

Mkutano utakuwa na vipindi vya warsha mbalimbali:

- Ukimbizi na uhamaji
- Uinjilisti
- Maisha katika ukamilifu wake
- Utofauti katika mifumo

## MAONESHO

- Vijana
- Haki za kijinsia
- Misioni kutoka pembezoni

(CHANZO: WCC)

# Ifahamu safari ya Misioni kiekumene

**Mkutano wa Misioni wa Dunia awali ulijulikana kama Kamisheni ya IMC - 'International Missionary Conference'; chombo cha kiekumene cha kikriso kilichosaidia kujenga ushirikiano katika kazi za misioni baina ya madhehebu katika karne ya 20. Je tangu kuanzishwa chombo hiki kimefanya mikutano mingapi? Ifuatayo ni idadi na mahali ambapo mikutano mingine ya aina hiyo ilifanyika.**

**Edinburgh, Uingereza**

Mkutano wa Kwanza wa Kimataifa wa Misioni ulifanyika Edinburgh, Uingereza mwaka 1910 na kuhudhuriwa na washiriki 1,200. Mwaka 1921 International Missionary Conference (IMC) iliundwa na kilisisitiza majadiliano yanayojenga umoja wa wakristo.

**Jerusalem, Israel**

Mkutano wa Pili ulifanyika 1928 Jerusalem, Israel na kusisitiza kuhusu Misioni na Ufalme wa Mungu na uhusiano kati ya ukristo na dunia inayoshindana.

**Tambaram, India**

Mkutano wa Tatu ulifanyika Madras, Tambaram, India, mwaka 1938 na kauli mbiu ilikuwa kanisa kama wakala wa misioni na kuhusianisha ukaribu uliopo kati ya amani ya dunia na uenezi wa injili duniani. Suala la kuwa na midahalo ya kidini lilijitokeza Tambaram, India

**Whitby, Canada**

Mkutano wa Nne ulifanyika Whitby, Canada mwaka 1947, uliotafakari mabadiliko makubwa yalishoshtua baada ya Vita vya Pili vya Dunia. Kauli mbiu ikawa "Ushirikiano katika Utiifu."

**Willingen, Germany**

Mkutano wa Tano ulifanyika Willingen, Germany, mwaka 1952. Mkutano ulisisitiza kwamba kitovu cha kazi ya kanisa ni misioni. Ulifafanua kwamba misioni ni misioni ya Mungu (missio Dei) pamoja na kwamba ni wajibu mmoja wapo wa Kanisa.




**Washiriki wa Mkutano wa 13 ulifaonyika Ugiriki 9 hadi 16 Mei, 2005 wakiandamana wakiwa wamebeba msalaba. Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa mkutano huo kufanyika nchi ya waumini kwa Orthodox.**

**Achimota, Ghana**

Mkutano wa Sita ulifanyika Achimota, Accra, Ghana mwaka 1957–58. Majadiliano ya Achimota yalileta mageuzi makubwa kwa kuwa mkutano ulijadili namna ya kuunganisha majukumu ya misioni kiekumene chini ya Kamisheni ya IMC na kazi zilizokuwa zikifanywa na Baraza la Makanisa Duniani (WCC). Matokeo yake uamuzi wa kuyaunganisha majukumu yaliyokuwa chini ya Kamisheni ya Misioni (CWME) na WCC.

**New Delhi, India**

Mkutano wa Saba ulifanyika New Delhi, India mwaka 1961 na kuweka uzito mkubwa kwamba misioni iendeshwe kiekumene kutokana na ushiriki mpana wa madhehebu yakiwemo makanisa ya Orthodox na Kanisa Katoliki ambao wanashiriki kama watazamaji (observer).

Mwaka 1961, IMC iliunganishwa na WCC na kuanza kuandaa Mikutano ya Misioni ya Dunia.

Kamisheni ya Misioni na Uinjilisti ya Dunia katika Baraza la Makanisa Duniani (WCC) ilirithi wajibu wa kuandaa mikutano ya Misioni ya Dunia toka Baraza la Kimataifa la Misioni (International Mission Council - IMC) lililoundwa na Mkutano wa kwanza kimisionari wa kimataifa uliofanyika Edinburgh, Uingereza mwaka 1910.



**Rais Kwame Nkrumah wa Ghana alihudhuria ufunguzi wa Mkutano wa CWME uliofanyika Achimoto, Ghana.**

**Mexico City**

Mkutano wa Nane ulifanyika Mexico City mwaka 1963, kauli mbiu ilikuwa "Misioni katika mabara sita." Katika mkutano huo mtazamo wa misioni uligeuzwa kwamba iwe ni kwenda au kutoka kote kote na si kutoka magharibi kwenda mashariki au kaskazini kwenda kusini peke yake.

**Bangkok, Thailand**

Mkutano wa Tisa ulifanyika Bangkok, Thailand mwaka 1972–73. Mkutano ulikuja na dhana pana ya "Wokovu leo."

**Melbourne, Australia**

Mkutano wa 10 ulifanyika Melbourne, Australia mwaka 1980, na ulifanyi kazi kauli mbiu "Ufalme Wako uje."

**San Antonio, Texas**

Mkutano wa 11 ulifanyika San Antonio, Texas mwaka 1989. Kauli mbiu ilitoka katika sala ya Bwana, "Mapenzi yako yatimizwe: Misioni kwa njia ya Kristo."

**Salvador da Bahía, Brazil**

Mkutano wa 12 ulifanyika Salvador da Bahía, Brazil mwaka 1996 Uliotafakari Injili na utamaduni.

**Athens, Greece**

Mkutano wa 13 ulifanyika Athens, Greece Mei 2005 na mkazo ulikuwa kutumia misioni ili "kuponya na kupatanisha".

**Arusha, Tanzania**

Mkutano wa 14 wa Misioni wa Dunia umefanyika tena Afrika Arusha 8 - 13 Machi 2018 chini ya kauli mbiu, ***"Kuenenda kwa Roho: Wito wa Kuwa Wafuasi wa Mabadiliko".***

(CHANZO: © WCC)

# Afrika ni kinara kwa kazi za misioni

**Baraza la Makanisa Duniani limeandaa mkutano wa Misioni wa Dunia *(World Council of Churches - WCC)* utakaofanyika Arusha 8 hadi 13 Machi, 2018. Je unaelewa nini kuhusu mkutano huo. Yafuatayo ni mahojiano yaliyofanyika kati ya MWANDISHI WA WCC na DKT. AGNES ABUOM, kutoka Kanisa la Anglican Kenya, ambaye ni kiongozi wa vikao vya Kamati Kuu WCC:**



Dkt. Agnes Abuom Mwenyekiti Vikao vya Kamati Kuu ya Baraza la Makanisa Duniani (Chanzo: (c) WCC).

**Swali: Unaelezeaje historia fupi ya Mkutano wa Misoni wa Dunia yaani kwa kifupi CWME?**

**Dkt. Abuom:** Je ulifahamu kwamba tafiti na takwimu za dini zimebaini kuwa Afrika na nchi nyingine za kusini (mwa dunia) ni kitovu cha Ukristo? Kwa mara ya kwanza Afrika ilikuwa mwenyeji wa mkutano wa Misioni wa Dunia (CWME) miaka 60 iliyopita uliofanyika Achimota, Ghana mwaka 1958. Nchi ya Ghana ilipata Uhuru mwaka mmoja kabla ya mkutano huo kufanyika. Ulikuwa ni wakati nchi nyingi za Afrika zilikuwa katika vuguvugu la kupata uhuru toka utawala wa kikoloni. Kadiri makanisa ya Kiafrika yalivyozidi kulelewa na vyama vya misioni, pia ulikuwa ni wakati bara la Afrika lilikuwa likipita hali ya matumaini; Afrika ilikuwa ikipitia katika hali ya matumaini licha ya kuganga majeraha, mifarakano, kutengana kwa jamii na kutokuwepo kwa mifumo ya haki kijamii, kiuchumi na kisiasa.

**Swali: Kwa nini unaamini Mkutano wa 2018 wa Misioni wa Dunia una umuhimu katika historia?**

**Dkt. Abuom:** Eneo la mkutano litatoa fursa kuona hali halisi ya jamii ya Afrika ilivyo na taabu, hasira na kusherehekea licha ya changamoto katika kazi za misioni kiekumene siku hizi. Mikutano iliyotangulia nayo ilikabili masuala ya wakati wake kama ubaguzi wa rangi, amani, ushirikiano na upatanisho. Kwa mara nyingine tena Afrika inapaswa kurudi ili kujipanga vema zaidi katika suala la *imani ya Kikristo* na kujiuliza je, ***wito wa kuwa "ufuasi wa mabadiliko"*** uko katika kuwa na uwezo wa kuyabadilisha maisha ya watu kote duniani au ni kuwaacha baadhi ya watu wabaki utumwani?

**Swali: Kwa nini mkutano huu umefanyika Afrika?**

**Dkt. Abuom:** Mahali pa mkutano panatukumbusha *makutano* ya imani mbalimbali barani Afrika: Ukristo, Uislamu na dini za jadi za Kiafrika. Ni mahali panapohuisha roho ya kutaka mabadiliko na haja ya kuwa na dunia yenye mtazamo mbadala, unaolenga kuwa na mfumo wa kiuchumi na kisiasa ulio rafiki kwa watu, uliokolezwa na tunu zinazothamini uhai na mambo ya kiroho.

Pamoja na kutoa viongozi katika Misioni kiekumene duniani, michango ya Afrika inabaki kuwa ni ya kipekee sana kwa kuwa inasisitiza "utu" au "ubuntu" jambo linalotamka kwa dhati kwamba *kila mtu ni sura na mfano wa Mungu* bila kuwa na ubaguzi kijinsia, kicheo, kiwadhifa au utofauti wa rangi. Pia ni fursa ya kushirikisha wengine utamaduni unaojali utu na kukarimiana.

**Swali: Changamoto zetu ni zipi?**

**Dkt. Abuom:** Ukishakubali kwamba sisi kama wakala tumeitwa na Kristo ili kutatua migogoro mikubwa na midogo; biashara ya binadamu na wakimbizi waliolazimishwa kukimbia makwao; ubaguzi wa rangi wa aina zote pamoja na umaskini uliokithiri, ndipo tunapotakiwa kufikiri upya na kujenga upya dhana kuhusu wito wetu na maana ya ufuasi. Hii itasaidia kugeuza simulizi ya Afrika zionekane njema; kwamba ni za jamii iliyojaa amani, utulivu, heshima na usawa.

**Swali: Je unaweza kutafakari kidogo kuhusu kauli mbiu ya mkutano isemayo: *"Kuenenda kwa Roho: Wito wa kuwa wafuasi wa mabadiliko?"***

**Dkt. Abuom:** Kauli mbiu hii imehifadhi mwendelezo wa hamu ya watu wengi wanaotaka pawepo uhuru wa kweli na ukombozi barani Afrika na duniani kwa ujumla. ***"Ufuasi wa mabadiliko"*** ni jambo la msingi katika kuhuisha dhana na desturi ya kuwa mtumishi anaye eneza ***Habari Njema*** kwa kutumia mifumo na michakato inayohuisha malezi na maisha ya watu. Kwa hiyo ***"ufuasi wa mabadiliko"*** katika karne ya 21 ni kule kukubali mwaliko kwa kuwaelezea wengine habari zako na wao wakusikilize, waelewe na kushiriki kutenda uliyoyapata kwao kwa habari za kiroho, habari kuhusu jitihada za kutafuta haki, utu na heshima.

**Kwa maelezo zaidi kuhusu Mkutano wa Misioni wa Dunia fungua tovuti:** http://www.oikoumene.org/en/press-centre/events/conference-on-world-mission-and-evangelism-moving-in-the-spirit-called-to-transforming-discipleship/

# Kauli mbiu ya Mkutano wa Misioni wa Dunia

## *"Kuenenda kwa Roho: Wito wa kuwa wafuasi wa mabadiliko"*

**Na Dkt. Rogate Mshana**

Kauli mbiu ya Mkutano wa Baraza la Makanisa Duniani ukaofanyika Machi 2018 Ngurdoto, Arusha ni ***"Kuenenda kwa Roho: Wito wa kuwa wafuasi wa mabadiliko"*** *(Moving in the Spirit: Called to Transforming Discipleship)* kama alivyotafsiri Mkuu wa Kanisa letu Askofu Dkt. Fredrick O. Shoo katika salamu zake za mwaka 2018 kwa Kanisa.

Neno hili anasisitiza Mkuu kuwa, "linatutaka sote tunaomwamini Bwana Yesu na kuenenda katika Roho, tuwe waliobadilika na kuwa chachu ya mabadiliko katika jamii zetu."

Mkutano huo una sifa bainifu nne ambazo ni chembechembe za umisioni, uekumene, ujana na Uafrika. Ni mkutano unaofanyika mara moja kila miaka 10 ili kutafakari ishara za nyakati na ulimwenguni katika nyanja za upatanisho, haki za binadamu, amani na uumbaji wa Mungu.

Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji kwa kuwa ni nchi ya amani, isiyo na ubaguzi, madhehebu na dini mbalimbali hushirikiana na Ukristo unakua haraka.

Lengo la mada hii ni kutoa ufafanuzi wa kauli mbiu ya mkutano kwa mujibu wa Kamati ya Maisha ya Kiroho ya mkutano huo wa kipekee.

**SEHEMU YA KWANZA** ya Neno kuu inatoka Wagalatia 5:25, ***"Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho."*** Kila tunaposoma ishara za nyakati kwa pamoja ni dhahiri kuwa licha ya adha ya migawanyiko ya binadamu katika ulimwengu huu, kuna dalili nyingi za uwepo wa Roho Mtakatifu anayetupa uzima na matumaini. Afrika ni mahali ambapo Roho Mtakatifu anavuvia uzima katika Kanisa. Kuenenda kwa Roho kunaashiria dhana ya safari ya hija takatifu (pilgrimage) ya waumini wote wakiongozwa na Roho Mtakatifu. Hii ni safari inayobainishwa na matumaini ya kuwepo kwa ulimwengu uliobadilika na kuwa na haki, amani na uamsho katika



**Dkt. Rogate Mshana, Mwenyekiti Kamati Mwenyeji Mkutano wa Misioni wa Dunia.**

Kristo. Kwa hiyo, neno hili kuu ni ujumbe wa kinabii dhidi ya mikanganyo iliyopo katika ulimwengu wa sasa.

**SEHEMU YA PILI** ya Neno kuu ni wito wa kuwa wafuasi wa mabadiliko. Tumepewa wito wa kuwa wafuasi wa Yesu wa Nazareti ambaye tunamshuhudia na kumhubiri tunaposafiri katika Roho. Tunaelewa dhana ya "wafuasi wa mabadiliko" katika sehemu mbili zinazohusiana. **Kwanza** tunaitwa kuishi maisha yanayobadili ufuasi kama unavyojulikana. Ufuasi huu ni ule unaowabadili kila wakati wafuasi wanapojifungua zaidi kumpokea Kristo abadili maisha yao na kwa ajili hiyo jamii ya kikristo kubadilika. Ufuasi wa aina hii ni ule ulio na ari ya kubadili ulimwengu uliojaa udhalimu, maumivu na mateso. Kwa hiyo, **pili** ufuasi wenyewe unahitaji kubadilishwa. Ufuasi hueleweka katika maana ya kuwa katika uhusiano wa upendo, yaani upendo wa kirafiki na Yesu Kristo. Ingawa huu ndio ukweli bayana, ufuasi unaosisitizwa katika mkutano huu sio wa kimahusiano tu bali ni ule wa kuendelea kufanya kazi ya Missioni ya Kristo ulimwenguni. Kumjua Kristo ni kufuata yale aliyofanya. Hiki ni kitu ambacho Wanatheologia wa makanisa ya mwanzo waliita "theosis" yaani tunashiriki katika asili ya Mungu tunaposhiriki katika misioni yake. Ufuasi basi, ni kama Papa Francis alivyosema kwamba ni ***"Ufuasi wa kimisionari"*** *(missionary discipleship)*. Unatuita tumshuhudie Yesu na Ufalme wa Mungu aliouhubiri na inapofaa kulitangaza Jina lake na Injili pia. Unatuita kufanya Uinjilisti kwa kufuata jinsi Kristo alivyofanya.

**Pili** maana ya ufuasi ni wito wa kuwa wafuasi ambao wapo tayari kila wakati kubadilika, binafsi na kijamii katika kumfuata Yesu. Ufuasi unatupa ari ya kuwepo katika safari ya kiroho ambayo itaendelea kutupa changamoto na kutufinyanga kuwa watu wanaomtafakari Yesu Kristo katika matendo yetu, maneno na tabia. Ufuasi hutupa ari ya kuwa katika sala na vitendo vinavyobadili tabia, mioyo yetu na kutujenga ili kupata nguvu na ujasiri wa kutuwezesha kuishi maisha ya ushuhuda wa Kikristo.

**Tatu,** tunaitwa kuwa wafuasi wanaobadilika wenyewe na kwa ajili hiyo tumepata neema ya kuifanya Misioni ya utatu wa Mungu, tukifanya kazi kwa pamoja katika kuleta uzima, kuishi kufuata maadili ya Ufalme wa Mungu na kushughulika na Misioni inayotoka pembezoni (mission from the margins) kwa wale waliotengwa na kunyanyaswa katika jamii. Katika ulimwengu ambapo udhalimu umeshamiri, ambapo ubaguzi wa rangi na chuki vimezidi, ambapo mateso yameenea na kuogopesha, ufuasi ni wa gharama sana. Ufuasi ni wito wa kuiweka theologia ya msalaba katika vitendo. Unatutaka kutumia nguvu zetu na hata kutoa uhai wetu kuleta mabadiliko yanaoahidiwa na Ufalme wa Mungu. Ishara za nyakati zilizopo sasa ni kama hizi: kuishi katika ulimwengu wenye ugomvi, ukatili na kutokuwa sawa kiuchumi, umaskini, ubaguzi wa kijinsia na kijamii; Afrika na ulaya na sehemu zingine ulimwenguni kukabiliana na wakimbizi na utumwa wa kisasa. Mengine ni ukuaji wa teknolojia na maadili yake; dini zenye misimamo mikali kuathiri watoto. Pia Kanisa linakosa kuaminiwa kutokana na watumishi wake na kuhitaji uamsho. Umisioni kuzidi sehemu nyingine na kupungua mahali pengine ni changamoto; ukuaji wa Injili ya utajirisho una changamoto kwa Kanisa ulimwenguni. Pia masuala ya usomi unaohimiza ubinafsi na kudhoofisha ushirikiano kijamii. Mwisho ishara ya binadamu kuharibu uumbaji wa Mungu (Mwanzo 1: 26ff).

Ina maana gani kwetu kama watu binafsi na makanisa yetu kubadilishwa na nguvu za Roho Mtakaifu? Itakuwa na maana gani kujiunga na Roho katika kuleta mabadiliko katika ulimwengu uliovunjika? Haya ndiyo maswali ambayo mkutano huu utajadili.

Mkutano utakuwa pia na Ibada, masomo ya Biblia, kongamano, warsha na maonesho.



**Baadhi ya watumishi wa WCC na wajumbe wa kamati ya maandalizi ya mkutano wakipata maelezo kutoka hoteli ya Ngurdoto ambayo ni eneo la mkutano.**

# Kamisheni ya Misioni inaunganisha wote

Metropolitan Dkt. Mor Geevarghese Coorilos

Kamisheni ya Misioni na Uinjilisti ya Dunia katika Baraza la Makanisa Duniani (WCC) ilirithi wajibu wa kuandaa Mikutano ya Misioni ya Dunia toka Baraza la Kimataifa la Kimisionari (International Missionary Council - IMC) lililoundwa na Mkutano wa kwanza kimisioni wa kimataifa uliofanyika Edinburgh, Uingereza mwaka 1910.

Mwaka 1961, IMC iliunganishwa na WCC na kuanza kuandaa Mikutano ya Misioni ya Dunia katikati ya mihula ya mikutano mikuu ya WCC. Na Mkutano wa mwisho yaani wa 13 wa Misioni wa Dunia ulifanyika Athens, Greece mwaka 2005.

Mkutano wa kukumbuka miaka 100 tangu mkutano wa Edinburgh, ulifanyika mwaka 2010 kwa kuandaliwa na taasisi mbalimbali za kiekumene na za misioni. Hivyo basi Mkutano wa 14 wa Misioni wa Dunia utakaofanyika Arusha una umuhimu mkubwa kihistoria maana unaendeleza mapokeo ya tangu mkutano ule wa Edinburgh mwaka 1910.

Tuwapo Arusha tutashirikiana kujadili masuala mbalimbali ya misioni na kisha kutafakari na kubuni mbinu mpya ili kutekeleza kwa dhati misioni ya Mungu kwa mtazamo uliopo sasa.

Mkutano wa Arusha umeandaliwa uwe ni makutano ya misioni Kiafrika. Mara ya kwanza IMC iliandaa Mkutano wa Misioni wa Dunia barani Afrika ilikuwa mwaka 1958 mjini Achimota, Ghana. Miaka 60 baadaye, Mkutano wa Misioni wa Dunia unarudi Afrika ambapo sasa Afrika imekuwa kitovu cha Ukristo duniani na mahali ambapo roho anavuma kwa kishindo kikubwa. Kwa hiyo, kauli mbiu - ***“Kuenenda kwa Roho: Tumeitwa kuwa wafuasi wa mabadiliko”*** - ina dokeza Uafrika ambao washiriki watakaofika tunataka kujifunza kwa kuuchunguza kwa karibu.



Metropolitan Dkt. Mor Geevarghese Coorilos,
Mwenyekiti Kamisheni ya Misioni na Uinjilisti ya Dunia WCC.

Ni matumaini yetu kwamba mkutano wa Arusha utakuwa ni makutano ya kweli ya Kiafrika ukibubujika utajiri mwingi wa kitheolojia na kitamaduni.

Mikutano ya Misioni ya Dunia ni fursa kwa Kanisa duniani na vyama vya misioni kuishi ombi la kikuhani aliloomba Yesu Kristo kwamba ***“Wote wawe na umoja ili ulimwenugu upate kusadiki,”*** (Yohana 17:21).

Ni fursa kwa makanisa kuwa pamoja ili kuelezea umoja wao ulivyo katika kushuhudiana. Na hili lilikuwa lengo la kuunganisha IMC katika WCC lililoasisiwa na viongozi waliotutangulia miaka 60 iliyopita. Kwamba umoja na Misioni yalipo unganishwa na WCC ni kwa kuwa ni mambo yanayo kwenda pamoja.

Tunatumaini kwamba tutakapo tafakari na kwa njia ya maombi ya pamoja na kujadili mada chini ya kauli mbiu ***“Ufuasi wa mabadiliko”*** kutatujiingiza katika hija itakayoongozwa na Roho kuelekea haki na amani huku na sisi wenyewe tukibadilishwa - ambapo kupitia sisi na dunia tunamoishi nako kutakuwa na mabadiliko makubwa.

Ombi langu maalum ni kuwaalika tuje pamoja katika mkutano huu tukiwa tumeweka wazi mioyo yetu ya kiekumene na kunuia kwa dhati kutambua na kujifunza ni nini wito wetu wa misioni ya Mungu kwa sasa. Tujiweke tayari kusikiliza na kushirikishana na ndugu zetu wa kiume na wa kike kutoka pande zote za dunia. Tujiandae kupokea vionjo vya lafudhi ya Roho Mtakatifu vinayoweza kusukumwa na kupewa nguvu kupitia misioni ya Roho Mtakatifu. Kutokana na uhaba wa raslimali fedha hatukuweza kuwa na washiriki zaidi ya watu 1,200 waliokwisha pokea mwaliko. Lakini nina hakika kwamba kwa namna mbalimbali jumuiya na jamii itapata taarifa kuhusu mahangaiko, matumaini ya maisha na kuwapelekea walio nyumbani matokeo ya mkutano huo.

Tushiriki vizuri vipindi vyote vya mkutano ili kujenga jamii ya mabadiliko kimisioni. Kamisheni inatoa shukrani za dhati kwa kukubali kushiriki katika hija hii ya kimisioni ***- “Kuenenda katika roho: Tumeitwa kuwa wafuasi wa mabadiliko.”***

**CHANZO: WCC**

# GETI ni nini?

GETI ni ufupisho wa maneno *Global Ecumenical Theological Institute* (GETI). Ni programu ya muda mfupi ya wanafunzi wa theologia kutoka madhehebu mbalimbali chini ya mpango uliobuniwa na Baraza la Makanisa Duniani (WCC).

Kwa mara ya kwanza GETI ilifanyika sambamba na Mkutano Mkuu wa 10 wa WCC uliofanyika Busan, Korea ya Kusini mwaka 2013.

GETI itakutana tena kabla ya Mkutano wa 14 wa Misioni wa Dunia. Mafunzo yatafanyika Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (TUMA) na baada ya hapo wajumbe wa GETI 2018 watashirikishwa katika matukio na ratiba ya Mkutano wa Misioni wa Dunia.

Pamoja na mambo mengine washiki wa **GETI 2018 Arusha** watashirikishana uzoefu wa kazi ya Misioni katika utamaduni na maudhui au mazingira yao ***waliyoitwa na kuenenda katika Roho ili kubadili dunia.*** Wanafunzi hao kabla ya kukutana Arusha walipokea mafunzo kwa njia ya mtandao. Wakiwa nchini wanafunzi watafanya ziara za mafunzo kabla ya kuhudhuria mkutano wa Misioni wa Dunia.

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA






Askofu Liverson Mng'onda (pichani kushoto) wa Kanisa la Anglican Kenya aliongoza ujumbe wa watu 16 wakiwemo wachungaji na watendakazi wa Idara ya maendeleo wa Kanisa hilo. Walionana na kupata maelezo toka uongozi wa KKKT 14 Februari 2018 na waliweza kutembelea eneo la Longido. Pichani kulia ni ujumbe huo wa Kanisa la Anglican wakijitambulisha kwa watumishi wa Ofisi Kuu ya KKKT 14 Februari 2018.




**PICHA ZOTE NA: Elizabeth Lobulu**

Mch. Anza Amen Lema, Mratibu wa Vijana KKKT, hivi karibuni aliweka wakfu pikipiki mbili kwa ajili ya Kurugenzi ya Afya katika Ofisi Kuu ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.

Kaimu Mkurugenzi wa Afya KKKT, Dkt. Z. Mmbando, alisema wakati wa hafla iliyofanyika tarehe 15 Februari, 2018 kwamba vyombo hivyo vitatumiwa na Kitengo cha Tiba Shufaa (Palliative Care) eneo la manispaa na Halmashauri ya Arusha (DC).



KKKT iliandaa hafla ya kifungua kinnywa kuwapongeza madaktari watano waliohitimu mafunzo yao mwishoni mwa 2017.

# Viongozi wa Kanisa Afrika mjitathmini - wito



Wajumbe wa warsha wakiongozwa na Rais wa FMKD, Askofu Mkuu Dkt. Musa Filibus, walipata wasaa kutembelea Usharika wa Kimara, Mbezi Beach na Kijitonyama. Katika Usharika wa Kimara Rais wa FMKD Askofu Mkuu Dkt. Musa Panti Filibus alibatiza watu 16 wakiwemo wazima na watoto waliotoka dini nyingine.



Askofu Dkt. Alex Malasusa aliyemwakilisha Mkuu wa KKKT katika warsha, akiongoza wajumbe wengine kuagana na Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhe. Mwigulu Nchemba, aliyefika Ukumbi wa Luther House kusalimu wajumbe wa warsha.



Picha ya pamoja wakati wa ufunguzi wa warsha ya FMKD iliyofanyika Dar es Salaam.

**Na Elizabeth Lobulu**

Rais wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD), Askofu Mkuu Dkt. Musa Panti Filibus, amewahimiza viongozi wa makanisa barani Afrika kujitathmini kwanza kabla ya kutoa sauti ya unabii kwa lengo la kukosoa mamlaka nyingine. “Haitoshi kukinzana na mfumo uliopo bila kutoa mbadala kwa unayokosoa.”

Askofu Dkt. Filibus alisema hayo wakati wa ziara yake ya kwanza nchini Tanzania tangu awe Rais wa FMKD. Alihutubia warsha iliyoandaliwa na FMKD jijini Dar es Salaam kuhusu mbinu za kupambana na umaskini na uonevu wa kiuchumi Afrika iliyofanyika 10 - 13 Oktoba 2017.

Katika mahojiano maalumu na mwandishi huyu Askofu Mkuu Dkt. Filibus alisema viongozi wa kijamii wataheshimu viongozi wa Kanisa endapo wataonesha msimamo ulio wazi, kuwa kielelezo na kuwa kama mwenge wa kuleta matumaini katika jamii. Alisema, “Tukifanya hayo tunapokabili miundo kandamizi, walio nje watatuelewa na wakati mwingine hatutakuwa na haja ya kukemea au kuzungumza neno lo lote.

“Ili kanisa liwe wakala wa mabadiliko lenyewe linapaswa kuondokana na mateso katika jamii pamoja na matumizi mabaya ya madaraka.

“Hivyo Kanisa likitaka sauti yake iheshimiwe inapasa na lenyewe liweke mambo yake vizuri kwa kuwa na malengo yaliyo wazi na si kuburuzwa au kufuata mkumbo kwa kuwa Kanisa si kama mashirika mengine ya kijamii. Kanisa limeweka mizizi katika Maandiko. “Tunaelewa kwamba wokovu ni zawadi itolewayo bure kwa Neema na huo ndio msingi wa kuwako kwetu katika jamii na ndiyo agenda ya Kanisa.

“Kanisa halifanyi kazi zake kwa kuwa limepata maarifa fulani ya kisayansi. Japo kuna uzoefu wa maarifa kama hayo lakini uzoefu wetu ni kwamba ***wokovu hupatikana bure, uumbaji huuzwi, na binadamu hawauzwi.*** Tumejifunza mada kuhusu haya yote katika Mkutano wa 12 wa FMKD uliofanyika mwezi Mei, 2017 Windhoek, Namibia. Masuala hayo ni muhimu kwa Kanisa kama wakala wa mabadiliko na kusaidia upatikanaji wa haki katika jamii.

Rais wa LWF alikuwa Tanzania kwa ziara ya wiki mbili kuanzia 7 Oktoba 2017. Pamoja na mambo mengine alihutubia katika Kanisa Kuu la Azania Front wakati wa ufunguzi wa warsha ya FMKD iliyofanyika Dar es Salaam tarehe 8 – 13 Oktoba, 2017.

# Afrika iendeleze matengenezo ya Kanisa



Picha ya pamoja ya wajumbe wa Mkutano wa LMC uliofanyika Iringa 15 hadi 17 Oktoba 2018.

Rais wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani, Askofu Dkt. Musa Panti Filibus, ametaka Kanisa barani Afrika liendelee *kujitengeneza wakati wote* ili lidumu katika wito wa kueneza Injili na kutoa ushuhuda katika jamii.

Rais wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (LWF), Askofu Mkuu Musa Panti Filibus, alisema hayo alipokuwa akitoa mada kuhusu: ***'Matengenezo ya Kanisa kwa mtazamo wa kiafrika'*** katika mkutano wa 14 wa *Lutheran Mission Cooperation (LMC) Round Table* uliofanyika Iringa 15 hadi 17 Oktoba, 2017.

Alisema maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka 500 ya matengenezo ya Kanisa si matukio ya kawaida bali ni fursa adhimu ya kutathmini na inayotakiwa kuendelea kujadili kwa uaminifu ili kutambua nini wito au utumwe wetu toka kwa Mungu kwa sasa kama Kanisa. Tunapaswa kufanya yote kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu anayeanzisha na kuelekeza matengenezo ya Kanisa.

Wana matengenezo wa karne ya 16 waliona mwelekeo mbaya kwa vile Kanisa lilikuwa na tuhuma za rushwa na kuacha kuongozwa na Neno la Mungu; hivyo matengenezo ya Kanisa Afrika kwa sasa nayo yasimamie Neno la Mungu kama vile Mtume Paulo alivyosema katika Waefeso 4: 14.

Afrika inahitaji matengenezo lakini Kanisa lijue ni matengenezo ya kuelekea wapi na lengo lake ni nini. Matengenezo Afrika yanapaswa kujenga umoja katika kueneza ujumbe wa Neno la Mungu kwa watu na kwa kuwafundisha vizuri washarika Neno la Mungu. Maono na matendo yetu yakirandana ndipo tunaweza kuleta mabadiliko katika jamii.

# Uhusiano wa KKKT na Kanisa la Kilutheri Malaysia waanzishwa

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) mwezi Januari, 2018 lilipokea wageni wawili kutoka Kanisa la Kilutheri la Malaysia ambao walikuja kuanza mazungumzo ya kuwa na uhusiano na KKKT.

Wageni hao ni Mch. William Loh ambaye ni Mkurugenzi wa Misioni na Mch. Chandran Kulasekaran ambaye ni Mkurugenzi wa Misioni kwa ajili ya wale wanaoongea lugha ya Kingereza.

Baada ya ziara yao, KKKT ilituma ujumbe wa watu wawili kwenda Malaysia. Wawakilishi wa KKKT walikuwa ni Askofu Adam Michael, KKKT Dayosisi Mkoani Mara na Mch. Rohho ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Misioni na Uinjilisti, KKKT.

Ziara hizo ziko chini ya mpango wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (LWF) wenye lengo la kujenga ushirikiano baina ya makanisa katika nchi zinazoendelea (South-South) badala ya kuwa na mahusiano na Kanisa mama (North-South) tu.




**Mch. William Loh Basel (kushoto) wa Kanisa la Kilutheri Malaysia akifuatiwa na Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo, Mch. Chandran Kulasekaran na Mch. Lazaro Rohho, Naibu Katibu Mkuu Misioni na Uinjilisti KKKT. Wageni hao kutoka Kanisa la Kilutheri Malaysia walifika Moshi kuonana na Mkuu wa KKKT.**

# Uhusiano wa Kanisa la Kilutheri na makanisa mengine

**Tujadili tofauti zetu kwa kutumia na Neno la Mungu kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu katika kuyajua mapenzi ya Mungu na jinsi ya kuenenda, ili umoja unaompendeza Mungu na amani yake vitawale ndani ya Kanisa na ndani ya jamii.**

**Na Mchg. Dkt. Ipyana Mwamugobole**

Jambo la kihostoria lilitokea pale Walutheri na Wakatoliki kwa pamoja waliposheherekea miaka 500 ya matengenezo ya Kanisa jijini Wittenberg, Ujerumani mwaka 2017. Kuhusika kwa Wakatoliki, hasa Papa katika mwendelezo wa maadhimisho haya kuanzia Lund, Sweden mwaka 2016, kwaweza kushangaza wengi.

Hii ni kwa sababu matengenezo ya Kanisa yaliyoratibishwa na Luther yalienda sambamba na mgawanyiko na magomvi ndani ya Kanisa na jamii kwa ujumla. Walutheri na Wakatoliki hawakuweza kuabudu pamoja tena wala kuoana.

Kilichotokea ulaya baada ya hapo ni kwamba kibali cha Mlutheri kuishi mahali palipotawaliwa na Mkatoliki, au Mkatoliki kuishi mahali palipotawaliwa na Mlutheri, kilitolewa kwa sharti la mgeni huyo kuwapa wenyeji mali zake zote ama kwa hiari au kwa nguvu.

Hata hivyo maadhimisho ya mwaka jana na hata ya miaka ya hivi karibuni, yamekuwa tofauti sana na maadhimisho ya Matengenezo ya Kanisa yalipoanza miaka 500 iliyopita, ambapo ilikuwa mwanzo wa kuanzisha Kanisa la Kilutheri na kujitenga na Kanisa Katoliki na kuanza kueneza Neno la Mungu kwa kufuata ukweli wa Injili. Hata hivyo, historia inaonyesha jitihada za kurejesha umoja na amani kati ya makanisa ya Kilutheri na Katoliki zimekuwepo kwa miaka mingi.

Nchini Ujerumani, watawala wa sehemu mbalimbali walishiriki katika kulifikia lengo hili. Kwa mfano, mahali palipotawaliwa na Mkatoliki, Walutheri walianza kuruhusiwa ama kutumia nyumba za ibada za Wakatoliki au kujenga nyumba zao za ibada.

Tena Walutheri na Wakatoliki wakaanza kuoana. Hata hivyo uhuru, umoja na amani vilikuwa na mipaka; kwani mtawala wa mahali husika, ndiye alikuwa na maamuzi ya mwisho juu ya ustawi wa madhehebu mengine.



**Mchg. Dkt. Ipyana Mwamugobole.**

Matengenezo ya mahusiano yameendelea. Mfano, katika maadhimisho ya ***Ungamo la Augusburg*** mwaka 1980, watheologia wa Kilutheri na wa Katoliki walijadiliana na kuja na msimamo wa pamoja wakikaza kuwa Yesu ndiye msingi wa *Imani ya Kikristo.*

Mwaka 1983 katika kusheherekea miaka 500 ya kuzaliwa kwa Martin Luther, mjadala wa kimataifa ulio wajumuisha watheologia wa makanisa haya mawili, ulifanyika, ambapo kwa pamoja walisisitiza kuwa mafundisho ya Luther hayapaswi kupuuzwa.

Kumekuwapo pia mijadala mingine mingi kati ya watheologia wa makanisa haya mawili na kuja na andiko lenye maelezo yaliyokubaliwa na pande zote mbili juu ya maana halisi ya mafundisho ya Luther.

Katika sharika nyingi nchini Ujerumani kwa sasa, pamekuwepo uhusiano mzuri baina ya makanisa haya mawili kupitia matumizi ya pamoja ya nyumba za ibada, kupitia Juma la kujadili Biblia kiekumene; juma hili huishia na ibada maalum, yaani Wachungaji wa Kilutheri wanaongoza ibada kwenye sharika za Wakatoliki, na Wachungaji Wakatoliki wanaongoza ibada kwenye sharika za Walutheri.

Haya na mengine mengi, ni matokeo ya makubaliano yaliyofikiwa mwaka 2003 (Charta Oecumenica). Kuna mijadala mingi inaendelea inayolenga kujua si tu historia ya Luther, bali nini sababu ya kutengana na kipi kifanyike ili kutengana kusitokee tena. Hizi zote ni baadhi tu ya jitihada za kurejesha mahusiano baina ya makanisa haya mawili.

Mvuto au msisimko mkubwa wa maadhimisho ya mwaka 2016, ulisababishwa na msisitizo wa pamoja kati ya Walutheri na Wakatoliki wa kutambua mafundisho ya Luther kama ajenda za kiroho na kitheologia zenye kuleta changamoto kwa makanisa yote.

Makanisa haya mawili yanaona kuna mambo ya kujifunza kutoka kwenye mafundisho haya na kuyatumia katika kujitathmini kama Kanisa. Ndiyo maana kwa pamoja, wameendelea kushiriki mijadala, semina, na makongamano, kama mwendelezo wa maadhimisho haya. Pia viongozi wa ngazi za juu katika Kanisa Katoliki, wameendelea kutembelea miji mbalimbali ya Luther kama ishara ya ushirikiano huo.

Ni vizuri kuhitimisha kwa kusema jitihada za kurejesha mahusiano baina ya Walutheri na Wakatoliki barani Ulaya, si jambo jipya, na kwamba makanisa haya yanaona ni hatua muhimu na endelevu.

Hivyo Papa kuhudhuria maadhimisho ya siku ya matengenezo yaliyofanyika Sweden mwaka 2016, ni ishara na matokeo ya jitihada hizo.

Hata hivyo, si kila mtu anaunga mkono jitihada hizi, hasa hatua ya Papa kuhudhuria maadhimisho ya Sweden. Baadhi wanaona ni sawa na kusheherekea jeraha ambalo Wakatoliki walijeruhiwa na Luther.

Tunachojifunza ni kwamba amani ya Kristo na umoja unaompendeza Mungu ndani ya Kanisa, ni mambo ya kuenziwa, kwani ni moja wapo ya utume wa Kanisa.

Hivyo ni vema kujadili tofauti zetu na kuzishughulikia kwa mwanga wa Neno la Mungu, huku tukiomba uongozi wa Roho Mtakatifu katika kuyajua mapenzi ya Mungu na jinsi ya kuenenda, ili umoja unaompendeza Mungu na amani yake vitawale ndani ya Kanisa na ndani ya jamii zetu.

**Mwandishi ni mtumishi wa *United Evangelical Mission* (UEM), Ujerumani.**

# Kilele cha Kumbukumbu miaka 500 ya Matengenezo



Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) liliadhimisha kumbukumbu ya miaka 500 ya matengenezo ya Kanisa kwa ngazi zote tarehe 1 - 8 Oktoba 2017. Kilele kilikuwa tarehe 8. Dayosisi 25 za KKKT ziliwakilishwa katika Ibada iliyofanyika Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.



Kwaya nne ikiwemo ya watoto zilishiriki mashindano ya kwaya siku ya kilele cha kumbukumbu ya miaka 500 ya matengenezo ya Kanisa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira. Kushoto ni viongozi katika picha na wanakwaya wa Dayosisi Kusini Mashariki mwa Ziwa Victoria.



Kongamano la kilele cha kumbukumbu ya miaka 500 ya matengenezo ya Kanisa lilifunguliwa na Mkuu wa KKKT baada ya kupewa maelezo ya utangulizi na Makamu Mkuu Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Profesa Joseph Parsalaw, ambaye anaonekana akikaribisha washarika kabla ya kuanza Ibada.

Soma taarifa zaidi: http://www.elct.org/news/2017.10.004.html

# Washarika tusiwe vuguvugu - Mkuu




**Mnara wa Kilele cha Kumbukumbu ya Matenenezo ya Kanisa uliozinduliwa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira Oktoba 2017.**

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo, amewataka washarika wakae katika kweli ya Injili kwa kuwa binadamu anaokolewa kwa Neema ya Mungu hivyo hapaswi tena kukumbatia utumwa.

Askofu Dkt. Shoo alisema hayo alipokuwa mgeni rasmi na kiongozi wa Ibada ya kumbukumbu ya miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa ambapo kilele chake kiliadhimishwa na KKKT Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira tarehe 8 Oktoba, 2017.

Neno Kuu lilikuwa: ***"Tunaokolewa kwa Neema ya Mungu,"*** (Wagalatia 3: 10 – 12). Pia kulikuwa na mada ndogo tatu: "Wokovu si wa kuuza," "Wanadamu sio bidhaa ya kuuzwa" na "Uumbaji sio wa kuuzwa."

Alisema katika Injili ya Yohana, Yesu anasema ukiishafahamu kweli itawaweka huru. Na mwana akikuweka huru unakuwa huru kweli kweli.

Alisema Martin Luther alipata msukumo wa kuanzisha matengenezo ya Kanisa katika karne ya 16 baada ya kutafakari mafundisho toka Wagalatia 3: 10 – 12. Haikuwa lengo la Dkt. Martin Luther kuondoka katika Kanisa Katoliki wakati ule. Yeye alitaka Kanisa lisimame katika ukweli wa Neno la Mungu kwamba mwanadamu kuhesabiwa haki kwa Neema na si kwa matendo.

"Tunasamehewa dhambi na kupokea wokovu kwa neema na kwa njia ya imani kwa Yesu peke yake. Lililo kuu ni kukaa katika Neno la Mungu linavyotufundisha na kubaki katika ukweli wake bila kuyumba.

"Kuna upotoshaji wa Neno la Mungu, ambapo wapo wanaofikiri kile alichokifanya Yesu pale msalabani hakitoshi bali lazima na sisi tuongezee kitu kidogo. Lakini sivyo ilivyo kwa jambo la wokovu wetu.

"Tumefika hatua ya kufanya mambo ya ushirikina kwa kukubali hirizi tukifikiri kwamba zitatupatia Neema ya Mungu; lakini Neno tulilosoma litukumbushe kwamba mambo ya kupotosha ukweli wa Injili hayakuanza leo.

Wakati wa Mtume Paulo kule Galatia, yalikuwapo mafundisho kwamba mtu ataokoka tu kwa kutimiza sheria yote. Paulo alikemea na kushangaa watu walivyoacha ukweli wa Injili ya Kristo na kugeukia Injili nyingine. Pia alifika hatua ya kuwaambia: "***Enyi Wagalatia msio na akili, ni nani aliywewaloga?"***

Ndugu zangu, kama leo Mtume Paulo angekuja atazame KKKT, aingie katika ibada zetu, asikilize mahubiri yanayotolewa na awaangalie baadhi ya washarika kwa jinsi wanavyo hangaika huku na huko ataona watu wenye mahangaiko kutoka kwa mtumishi mmoja au nabii mmoja hadi kwa nabii mwingine na wanao kwenda hata kwa waganga wa kienyeji. Sijui kama Mtume Paulo angeacha kutuuliza. ***"Enyi Walutheri ni ni nani amewaloga?"*** Nani amekwambia njia za ibada yenu haina utukufu, haina upako?"

**Ukitaka kujisomea mahubiri yote fungua http://www.elct.org/ news/ 2017.10.004.html**

# Dkt. Mwaikali awekwa wakfu Dayosisi ya Konde



**Askofu Dkt. Edward Mwaikali KKKT Dayosisi ya Konde**

Mchungaji Dkt. Edward Johnson Mwaikali aliwekwa wakfu 14 Januari, 2018 ili kuongoza Dayosisi ya Konde ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) kuchukua nafasi iliyoachwa na Askofu Dkt. Israel-Peter Mwakayolile ambaye amestaafu.

Mara baada ya kuwekwa wakfu na kusimika kuwa Askofu wa KKKT alimweka wakfu Mchg. Geoffrey Samwel Mwakihaba kuwa Msaidizi wa Askofu Dayosisi ya Konde.

Askofu Dkt. Mwaikali alizaliwa 16 Agosti, 1969 Wilayani Tukuyu, Mkoa wa Mbeya na alihitimu Shahada ya Elimu ya Dini yaani *Bachelor of Divinity* ya Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira ambako alisoma tangu 1994 hadi 1999. Baada ya kuhitimu alibarikiwa kuwa Mchungaji 2000 na alikuwa Mchungaji Kiongozi Usharika wa Katumba, Mkoani Katavi 1999 hadi 2000. Pia alikuwa Mchungaji katika Kanisa Kuu la KKKT Dayosisi ya Konde lililopo Tukuyu 2002 hadi 2003.


Askofu Mwaikali alikwenda Oslo kwa Shahada ya Uzamili katika Theologia (falsafa) ya Chuo cha Norwegian Lutheran School 2000 hadi 2002. Alikuwa Mratibu wa programu ya kuelimisha masuala ya Virusi vya Ukimwi Dayosisi ya Konde iliyojulikana kama *Local Community Capacity Building Project* 2004 hadi 2005. Kati ya 2006 na 2009 alikuwa Msaidizi wa Askofu Dayosisi ya Konde. Alichukua masomo ya Stashahada ya Juu ya Maendeleo ya Kiuchumi nchini Netherlands kutoka Chuo cha Hague Institute of Social Studies 2007 hadi 2008. Kati ya 2010 na 2011 alichukua masomo ya Shahada ya Uzamili katika Uongozi *(Master of Science Degree in Organisation Development and Transformation)* ya Chuo cha Nairobi, Kenya kijulikanacho kama *United States International University.* Masomo yake ya Uzamivu yaani PhD aliyapata toka Chuo Kikuu cha Cebu Doctor's University kilichopo Philippines 2011 hadi 2015. Alikuwa mkufunzi katika Chuo Kikuu cha Katoliki Ruaha, Iringa yaani Ruaha Catholic University tangu 2012 hadi 2017.

Askofu Dkt. Mwaikali alioana na Joyce Mwakilembe na kwa pamoja wamejaliwa mtoto wa kiume mmoja na wa kike mmoja.

# Kissiri Askofu mteule Magharibi Kati

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania litazindua Dayosisi ya 26 mwezi Juni. Itaitwa Dayosisi ya Magharibi Kati.

Mkutano Mkuu wa kwanza wa Dayosisi teule ya Magharibi Kati (eneo lililokuwa Misioni la Tabora) uliofanyika 22 hadi 23 Novemba, 2017 ulimchagua Mchg. Isaac Kissiri Laiser kuwa Askofu wa kwanza. Viongozi wa dayosisi hiyo watawekwa wakfu mwezi Juni 2018.



Mch. Isaac Kissiri Laiser, Askofu Mteule, KKKT Dayosisi ya Magharibi Kati.

# Askofu toka Sweden atembelea KKKT



Mch. Dkt. Anneth Munga (kushoto), Askofu Dkt. Stephen Munga, Askofu Johan Tyrberg na mke wake Katharina.

Askofu wa Dayosisi ya Lund, Sweden hivi karibuni alitembelea Dayosisi ya Kaskazini Mashariki kwa lengo la kujenga mahusiano baina ya dayosisi hizo.

Askofu Johan Tyrberg na mke wake Katharina walitembea na kujionea kazi za kanisa katika sharika za mijini na vijijini ikiwa ni pamoja na Handeni katika eneo la Misioni Msomera ambapo kuna jamii ya Wamasai. Vikundi mbalimbali vya kwaya vilihusika katika ibada ambapo Askofu Tyrberg alibatiza watoto 12.

## Usajili wa makanisa utazamwe upya - wito

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dkt. Fredrick Shoo, ameomba Serikali itazame upya taratibu za usajili wa makanisa na taasisi za dini ili kuepusha kuenea kwa mafundisho potofu katika jamii.

Alitoa mfano jinsi mwaka 2000 Askofu Joseph Kibwetere wa Uganda alivyo waangamiza wafuasi wake 1,000 kwa kuwachoma moto baada ya kuwaaminisha kuwa mwisho wa dunia umefika.

# Kanda ya ziwa kupigania haki za albino

Viongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) kutoka Dayosisi tano za ukanda wa Ziwa Victoria wamekutana hivi karibuni mjini Karagwe kujadili mbinu za kuzuia mateso na mauaji ya albino.

Viongozi hao ni Maaskofu na Makatibu Wakuu wa Dayosisi za: Kaskazini Magharibi; Karagwe, Mkoani Mara, Mashariki mwa Ziwa Victoria na Kusini Mashariki mwa Ziwa Victoria.

Shirika la Kikristo linalo hamashisha, kutoa elimu na kutetea haki za albino liitwalo *'Under the Same Sun'* (UTSS) liliandaa warsha hiyo ya siku mbili chini ya uhisani wa Chama cha Danmission cha Denmark.

Pamoja na mambo wengine, warsha ilijadili mafanikio katika vita ya kuondoa ukatili kama vile ubaguzi, mauaji, bughudha na utekwaji wa watu wenye ualbino na changamoto zinazojitokeza.

Vitendo vya ukatili kwa watu wenye ualbino vimeshamiri katika ukanda wa Ziwa Victoria kuliko sehemu nyingine Tanzania.

Viongozi hao wa KKKT wameahidi kushirikiana na Shirika la *'Under the Same Sun'* ili kushirikisha watu wengi zaidi taarifa sahihi juu ya namna ya kutoa ulinzi kwa watu wenye ualbino na kusaidia kuhakikisha sera zinazohusu ulinzi na haki kwa watu wenye ualbino zinasimamiwa kuwawezesha waishi maisha yenye staha kama binadamu wengine.

# Mkurugenzi mstaafu Radio Sauti ya Injili aitwa mbinguni

Mkurugenzi wa mstaafu wa Radio Sauti ya Injili, Bw. Calvin Kimangano Lyaro, aliitwa mbinguni 06 Januari mwaka huu baada ya kuugua ugonjwa wa saratani kwa muda mrefu. Alizikwa nyumbani kwake katika Kijiji cha Rau, Wilaya ya Moshi vijijini tarehe 11 Januari, 2018.

Marehemu Lyaro aliyezaliwa 1942 alifanya kazi Radio Sauti ya Injili tangu 1967 hadi 2010. Alifanya kazi katika ngazi ya Ukurugenzi kutoka 1995 hadi alipostaafu mwaka 2010.

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Jamhuri ya Watu wa Kongo lilianzishwa baada ya viongozi wake kusafiri toka Lubumbashi hadi Moshi kwa kuwa wamevutiwa na mafundisho ya Neno la Mungu kupitia Radio Sauti ya Injili ambayo mawimbi ya sauti yake yalikuwa yakisikika Afrika Mashariki na ya Kati.

**Taarifa imetolewa na:**

Ofisi ya Katibu Mkuu, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).



Marehemu Calvin Kimangano Lyaro.

# Tambua na kabiliana na msongo wa mawazo

Na Shemeji Melayeki



Kuimba au kucheza ni kati ya mbinu za kukabiliana na msongo wa mawazo. Watumishi wa Ofisi Kuu ya KKKT wakimsifu Mungu wakati wa maburudisho ya mwishoni mwa 2017.

Msongo wa mawazo ni hali inayosababisha kukosekana kwa utulivu katika mwili na akili ya mwanadamu. Hali hii huathiri kemikali za mwili, hisia, na hata viungo vya mwili. Mwili au akili inashindwa kuhimili mikiki na changamoto za kila siku za maisha.

Utamtambua mtu mwenye msongo wa mawazo kwa vile anakuwa na hasira zisizokuwa na sababu; kichwa kinamuuma mara kwa mara; ana hofu isiyo ya kawaida; anakosa amani hata kama hakuna kitu alichokosea; ana anza kula sana au anakula kidogo sana au anakula kila wakati; uwezo wa kufikiri na kukumbuka unapungua; anasahausahau; anajutia maamuzi mengi aliyoyafanya; mwili unadhoofika; anakuwa dhaifu; anakuwa mpweke; anapata makunyanzi usoni isivyo kawaida na kutumia fedha bila mpango wo wote.

Mambo yanayosababisha msongo wa mawazo ni pamoja na matatizo binafsi kama kuugua muda mrefu; matatizo ya kihisia kama hasira au kutojikubali; matatizo ya kijamii kama upweke au matatizo sehemu ya kazi; matatizo ya kiuchumi na matatizo ya mahusiano katika familia.

Maendeleo yanapoongezeka tatizo la msongo wa mawazo linaongezeka. Saratani na magonjwa ya moyo yanasababishwa kwa kiwango kikubwa na msongo wa mawazo kuliko matumizi ya sigara na vyakula vyenye mafuta kwa pamoja.



Bw. Shemeji Melayeki.

Tafiti mbalimbali zinaonesha kwamba ajali nyingi za barabarani (madereva na waendao kwa miguu) zimechangiwa sana na msongo wa mawazo kwa kusoma ujumbe au kupokea simu wakiwa barabarani. Na watu wengi waliojinyonga walishindwa kukabiliana na msongo wa mawazo.

Imethibitika asilimia 61 ya watu, wanaugua nafsi kabla ya kuugua mwili. Uharibifu mwingi umesababishwa na watu kushindwa kukabiliana na msongo wa mawazo kazini, katika mahusiano au nyumbani. "Ni heri kuinama mwili kuliko kuinama nafsi"

Tunasoma Neno kwamba: "Muwe na hasira, ila msitende dhambi; jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka, (Waefeso 4:26); "…Huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu", (1 Petro 5:7) na katika Mathayo 11:28 tunaalikwa: "Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.

Mathayo 11: 29-30 Bwana Yesu anasema: "Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi."

**Mbinu za kuepuka msongo** wa mawazo ni pamoja na kupanga muda wako kila siku na kujifunza kukataa au kusema SIWEZI kwa mambo siyo muhimu kwako. Usitoe ahadi hewa wala usijitwike mzigo mzito sana kwa kufurahisha watu halafu uumie baadaye. Pumzika kila baada ya tukio kubwa.

Muda ukifika usiache kuchukua likizo hata kama kazi ni nyingi. Panga muda wa kufurahi, tembelea mbuga za wanyama, kutana na marafiki au tembelea sehemu za kumbukumbu, nk.

Panga kazi zako kwa kuweka vipaumbele; gawa kazi zingine kwa watu wengine, usijirundike kazi. Usiogope kukosea, ukamilifu sio utakatifu. Ila ni muhimu kukamilisha kazi uliyoanza kuifanya.

Wasaidie wasiojiweza, utagundua una sababu nyingi za kufurahi. Uwe muwazi na mkweli. Usihifadhi vitu moyoni. Ukiona dalili ya jambo litakalokutatiza baadaye tafuta suluhisho mapema, usisubiri moto utokee ndio ufikirie kuzima.

Tafuta namna ya kuwasamehe waliokuudhi na kuwaachilia moyoni mwako. Mtu akikukosea mwambie, ukikosea omba msamaha.

Jifunze vitu usivyovijua hasa kama ni vya muhimu kazini kwako na maishani mwako.

Usikope pesa kwa ajili ya matumizi au starehe. Pesa za mkopo zinatumika kutengeneza pesa. Ukikopa pesa kwa ajili ya mahitaji kama ada ya mtoto hakikisha una vyanzo vya mapato utakavyotumia kulipia mkopo.

Ishi maisha ya shukrani – kuna mambo mengi ya kumshukuru Mungu kuliko kuyahuzunikia yale machache yanayokwenda kombo. Tafuta utulivu unapotafuta majibu ya tatizo ulilonalo na ujijengee mawazo chanya. Mtu mwenye mawazo chanya huona mambo mazuri katika kila jambo gumu linalompata. Sema maneno ya kujitia moyo. Uwe nadhifu na kufurahi. Kila kitu kina mwisho hata kama hujui ni lini.

**Wasiliana na Shemeji Melayeki:**
**E-mail:shemeji.melayeki@gmail.com**
**Simu +255 714 548 565**

# FAHAMU HISTORIA FUPI YA KKKT

## Vyama vilivyo eneza Ulutheri

Mwanzo wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanganyika (baadaye Tanzania) kuwepo nchini ni mwaka 1887, Chama cha Misioni cha 'Berlin III' au 'Evangelical Missionary Society for East Africa' (EMS) kutoka Ujerumani kilipoanzisha kazi ya Injili Kigamboni, Dar es Salaam.

## Chama cha pili

Chama cha Misioni cha 'Berlin I', nacho kutoka Ujerumani, kiliingia Tanzania kikitokea Afrika ya Kusini na kuanza kazi Nyanda za Juu Kusini mwaka 1891 kilipoanzisha kituo au misheni sehemu iitwayo Ipagika au Pipagika (Wangemannshöhe) katika Dayosisi ya Konde kwa sasa.

Mwaka 1890, Chama cha Berlin III kilichukua sura mpya baada ya kubadili sera yake na kujulikana kwa jina la Bethel au 'Misioni ya Bethel'. Misioni hii ikafika sehemu za Tanga na kuanza kazi eneo la Mbuyukenda.

Baadaye Misioni hii iliamua kufikisha Injili ya Kristo nje ya mipaka ya Tanganyika. Wamisionari hao walipanga kwenda Rwanda kupitia Bukoba. Walipofika Bukoba wakafungua kituo mwaka 1910.

## Chama cha Leipzig

Chama cha tatu kufika nchini Tanzania ni Chama cha Misioni cha Leipzig, nacho kutoka Ujerumani. Kiliingia Tanganyika mwaka 1893 na kuanza kazi ya Misioni Kaskazini mwa nchi sehemu ya Kidia, Old Moshi na baada ya muda mfupi, kwa kushauriwa na Mtawala wa Kijerumani, Carl Peters, wakahamia Nkwarungo - Machame.

Pamoja na vyama vilivyoanzisha Ulutheri Tanzania, kuna mchango mkubwa wa vyama vya Misioni na makanisa toka Ulaya na Marekani tunayo endelea kushirikiana nayo kama: **cos, elcb, felm, dlm, danmission, sem, lmw, mew, nlm, nmz, bmw, uem, velkd, elca,** nk. Hakika Neno la Mungu linaendelea kufundishwa kwa upendo na kwa usahihi wakati wote huu.

## Vita za Dunia

Kanisa la Kilutheri nchini lilipita katika nyakati ngumu vipindi vya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia 1914 hadi 1918 na ya Pili 1939 hadi 1945. Chama cha Misioni Augustana kutoka Marekani pamoja na Walutheri kutoka nchi nyingine za Ulaya walitoa msaada sana wakati wamisionari wa Kijerumani walipoondoka.

## Makanisa Saba

Vyama vya Misioni viliendelea na kazi ya Injili na makanisa saba ya Kilutheri yakaanzishwa maeneo mbalimbali nchini. Makanisa hayo mwaka 1948 yaliunda Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Tanganyika. Tarehe 19 Juni 1963 makanisa yale saba yaliungana kuunda Kanisa moja la **KKKT** na makanisa yakageuka kuwa Dayosisi au Sinodi. Sinodi zikageuka kuwa Dayosisi na ifikapo Juni 2018 KKKT itakuwa na Dayosisi 26.

## Uongozi na usimamizi

Chombo kikuu cha maamuzi KKKT ni Mkutano Mkuu ambao hufanyika kila baada ya miaka minne. Halmashauri Kuu ya KKKT hukutana mara mbili kwa mwaka kwa vikao vyake vya kawaida. Wajumbe wa vyombo vyote hivi wanawakilisha Dayosisi zote za KKKT.

## Kazi za Umoja

Kanisa lina vituo na Ofisi Kuu ya Kazi za Umoja (Common Work). Ofisi Kuu ya Kanisa inaongozwa na Katibu Mkuu. Ina idara zifuatazo: Misioni na Uinjilisti; Mipango na Maendeleo; Fedha na Utawala; Huduma za Jamii, Kazi za Wanawake na Watoto. Pia kuna Kitengo cha Ukaguzi. Kazi ya Ofisi Kuu ya KKKT ni pamoja na ***kuratibisha, kuwezesha na kufanya utetezi*** kwa manufaa ya Kanisa zima.

KKKT ina taasisi na vituo vinavyotunza Kazi za Umoja:
**1.** Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira **2.** Seminari Ndogo ya Kilutheri Morogoro **3.** Kituo cha Redio Sauti ya Injili, Moshi. **4.** Shule za Msingi kwa watoto viziwi Mwanga na Njombe. **5.** Shule ya Sekondari kwa watoto viziwi Njombe. **6.** Miradi ya kuongeza kipato.

Pamoja na vituo vya Kazi za Umoja, Dayosisi zina hospitali 23 na zahanati / vituo vya afya 150. Dayosisi zote zina shule za msingi, sekondari na vyuo vya





**Mkuu wa KKKT,**
**Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo.**

ufundi na maarifa mbalimbali. Baadhi ya Dayosisi zina vyuo vikuu. Taasisi hizi hutoa huduma kwa watu wote bila ubaguzi.

Karibu kila dayosisi /taasisi zake/ idara zina miradi midogo midogo ya kuinua kipato; miradi ya maji salama, miradi ya ng'ombe wa maziwa, nk. Dayosisi nyingi zina miradi mikubwa na ya kati. Baadhi zimeanzisha mabenki au vyama vikubwa vya kuweka na kukopa (SACCOs).

## Kazi za Misioni

Kanisa limehisika na kusaidia uanzishwaji Kanisa la Kilutheri nchini Kenya, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Msumbiji, Malawi na Uganda. Pia linalea Kanisa la Kilutheri Zambia, Burundi na Rwanda. Ndani ya nchi maeneo ya Misioni ni Kigoma na Zanzibar.

## Ushirikiano na wengine

KKKT ni mwanachama hai wa: Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT); 'Lutheran Mission Cooperation' (LMC); Baraza la Makanisa Barani Afrika (AACC); Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (LWF) na Baraza la Makanisa Duniani (WCC).

## Ofisi zilipo

Ofisi Kuu ya KKKT ipo Arusha "Lutheran Centre", Barabara ya Boma mkabala na Posta Kuu. Senta hiyo ina hosteli kwa ajili ya watumishi na wageni wa Kanisa.

## Kwa maelezo zaidi wasiliana na

**Katibu Mkuu**
Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania
**S.L.P.** 3033, **Arusha**

**Simu:** 250 8856/250 8857/**Fax** 254 8858
**Barua pepe:** elcthq@elct.or.tz
**Tovuti:** www.elct.org
Au **Tovuti:** www.elct.or.tz

# Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania

**KKKT**


**ELCT**

tunawakaribisha washiriki wote wa

## Mkutano wa Misioni wa Dunia

8 - 13 Machi, 2018 Arusha, Tanzania

KARIBUNI



WELCOME

World Council of Churches